

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Ref.No.JA.9/259/01/A/60

25 Machi, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Katibu Wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi Wa Umma kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wataanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi kumi **(10)** kama ilivyoainishwa katika tangazo hili.

1.0 MWAJIRI: KATIBU MKUU WIZARA YA MAJI

1.0.1 MHAIDROJIA II (HYDROLOGIST II) NAFASI 6

1.0.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. kusimamia ujenzi na usimamizi wa ukarabati wa vituo vya hali ya hewa, vituo vya upimaji uwingi wa maji kwenye mitoni mabwawa na maziwa (discharge measurements);
- ii. Uchukuaji wa sampuli za mchanga unaosafirishwa kwenye mito (sediment sampling) na kuzitafsiri;
- iii. kufanya uhakiki wa takwimu (validation activities) wakati wa kuchakata takwimu.
- iiii. kuratibu ukusanyaji wa takwimu/taarifa zote za kihaidrolojia kutoka madakio na vidakio vya maji (catchments/sub catchments) na kuhakikisha takwimu zote kutoka kila kituo zinatumiwa makao makuu ya bonde kila mwezi na tarehe 15 ya kila mwezi unaofuata zinawasilishwa wizarani;
- iv. Kufanya uchunguzi wa awali wa shughuli zinazohusu vituo vya haidrolojia;

- v. Kutengeneza ramani za vidaka maji katika mabonde ya maji kwa kutumia njia ya geographical information system;
- vi. Kubadili takwimu za kina (water leves) cha maji mtoni kuwa wingi wa maji ya mito (discharge);
- vii. Kufanya ulinganifu wa mvua inayonyesha na mtiririko wa maji ya mvua (runoff) kwa kila siku na kwa kila siku kumi(10);
- viii. Kuchakata takwimu na kuona mpishano wa muda mrefu (shift behaviooron long term basis kwa kutumia duple mass curve);
- ix. Kuhakiki utunzaji mzuri wa kanzi data ya takwimu kulingana na miongozo na usimamizi wa rasilimali maji;
- x. Kukagua vifaa vya kazi za kihaidrolojia ofisini, stoo na katika vituo vya kihaidrolojia. xi. Kushiriki kuchukua, kuchambua na kutafsiri sampuli za mchanga unaosafirishwa kwenye mito;
- xii. Kukusanya, kuchambua na kutafsiri takwimu za maji kutoka vituo vya hali ya hewa na vya upimaji wa uwingi wa maji kwenye mito, mabwawa na maziwa;
- xiii. Kutayarisha na kurekebisha taarifa za kihaidrolojia zinazohitajika mara kwa mara katika ofisi za takwimu ya Taifa (NBS);
- xiv. Kushiriki katika kazi za usalama wa mabwawa; xv. Kushiriki kwenye kubainisha maeneo yanayoathiriwa na mafuriko; xvi. Kushiriki katika kutayarisha kielelezo cha mtiririko wa maji (rating curve equitation); na
- iv. kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

1.0.3 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Shahada ya Haidriolojia au Uhandisi wa Rasilimali za Maji kutoka vyuo vikuu vinavyotambuliwa na serikali. Wawe na ujuzi wa kutumia kompyuta.

1.0.4 NGAZI YA MSHAHARA TGS.D

1.0.5 FUNDI SANIFU MAABARA II (WATER LABORATORY TECHNICIAN II) - (NAFASI 3)

1.0.6 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Uchukuaji wa sampuli za maji na udongo kwa ajili ya upimaji; ii. Kufanya matengenezo ya vifaa vya maabara ya kawaida na ya dharula yanapohitajika;
- iii. Kufanya upimaji wa maji na udongo wa maeneo ya miradi na kuaandaa maelekezo ya matibabu yanayohitajika;
- iv. Ukusanyaji wa takwimu za hali ya maji na udongo zinazohitajika kwenye maeneo ya miradi;
- v. Kufanya uchunguzi wa sampuli za maji safi na maji taka kwa kutumia vifaa maalum (specialize equipment) kama vile Atomic Absorption Spectrophotometer, Kjeldah na mashine nyinginezo; vi. Kubaini viwango vya kiasi cha madawa yanayohitajika kwa kutibu na kusafisha maji (dosage);
- vii. Kufanya uchunguzi wa madawa ya kutibu na kusafisha maji; na viii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

1.0.7 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye elimu ya sekondari na cheti cha ufundi FTC au Stashahada ya Ufundi katika fani za Maabara za Maji kutoka katika chuo kinachtambuliwa na Serikali. Wawe na ujuzi wa kutumia kompyuta.

1.0.8 NGAZI YA MSHAHARA TGS .C

1.0.9 FUNDI SANIFU MAJI MSAIDIZI (ASSISTANT WATER TECHNICIAN II –CIVIL (NAFASI 1)

1.0.10: MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kufunga Pampu na injini za aina mbalimbali za maji na usafi wa mazingira;
- ii. Kufunga Pampu na injini za aina mbalimbali za maji na usafi wa mazingira kwa ajili ya kukidhi uendeshaji nadhifu endelevu na kuzuia uharibifu;
- iii. Kuhudumia uendeshaji wa pampu na injini za miradi ya maji; iv. Kufanya matengenezo ya kawaida ya vipindi kwa ajili ya kuzuia uharibifu wa pampu na injini kwa kufuata muongozo ya uendeshaji na matengenezo inapohitajika kwa dharura;

- v. Kutayarisha, kukusanya kutunza na kuziwasilisha takwimu za uendeshaji na matengenezo ya pampu na injini za miradi ya maji;
- vi. Kufanya kazi za ujenzi wa miundo mbinu ya maji ikiwemo ufungaji wa bomba na
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi

1.0.11 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne waliohudhuria na kufaulu mafunzo ya mwaka mmoja katika fani ya Maji kutoka katika Chuo cha Maji au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali ambao wana cheti cha Ufundi Daraja la III.

1.0.12 NGAZI YA MSHAHARA TGS.A

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45. ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyithibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
 - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
 - Computer Certificate
 - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)

- vi. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xi. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 07, Aprili , 2022.**

Muhimu: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**KATIBU OFISI YA RAIS
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA
S.L.P. 2320 DODOMA.**

- i. **Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <http://portal.ajira.go.tz/>**

(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa **‘Recruitment Portal’**)

BOFYA HAPA KUTUMA MAOMBI

- ii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na;

KAIMU KATIBU SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA